

## **Niwambiaje?**

Niwambiaje wenzangu, wa mbali na wa karibu?  
Mwendo nahisi uchungu, kuwa sina la kujibu  
Waliotujua tangu, mamwinyi katuhesabu  
Niwaambe nini leo, kwamba vyote katoweka?

Niwambiaje nambie, niseme wakasadiki?  
Kwa vichwa waitikie, kauli waiafiki  
Nisemalo waridhie, wasione unafiki  
Kwamba vyote twapoteza, vyakula vya asilia?

Niwambiaje watokao, kuno kunako mavumbi  
Waja toka maeneo, ya minazi na makumbi  
Matunda wafuatao, niambe tunazo kumbi?  
Hatuna zaraa ati, ni majengo yalokitwa?

Niwambiaje semeni, kwamba kuna maghorofa  
Na wengi ni masikini, walolimbuka ulofa?  
Maisha kwa kuwa duni, watembea japo kafa  
Chakula hawakimudu, kilimo ni marehemu?

Niwambiaje viazi, na parachichi hakuna?  
Tunaagiza ndizi, hatupandi tukavuna  
Niwambie siku hizi, mchanga sio hazina  
Twakumbatia usasa, unotukuza viwanda?

Niwambiaje yakini, soko halina perege?  
Vijaile gulioni, feki hata maharage  
Lipo tatizo majini, latowesha hata ndege  
Tuzile plastiki, badili ya kula nswi?

Niwambiaje kizuru, mikononi wana chondo?  
Niwapeni washukuru, nami nione uhondo  
Nafusini niwe huru, kufurahia matendo  
Nikashifu Afrika, kwa kuandama usasa?

**Malenga wa Vilimani**  
**(Kelvin Kombo Motuka)**  
**+254708867263**